MWONGOZO WA KUSAHIHISHA MTIHANI WA KITAIFA
2001
SWALI LA KWANZA
(a) (i) Mwanaume
Alikuwa na uwezo wa kuamua
Alistahili elimu ya juu
Ni mrithi
Ni kiongozi
Ni mwenye akili bora
Alidhaminiwa kuliko bora
Alidhaminiwa kuliko mwanamke
Ni mshauri

(ii) Mwanamke
Hatoi kupata elimu ya juu
Hastahili kurithi mali/ ufalme
Si kiongozi
Wa kuolewa
Ni chombo cha kutamanika
Ana akili dhaifu/ ana akili duni

(b) (i) Kwa nini mfalme aliwauliza wakwasi kwanza tafsiri ya kitendawili (alama 2)
Waliaminika au walidhaminiwa kuwa wenye ujuzi na maarifa
Waliheshimiwa/ Nasaba bora/ Ukoo mzuri
Walikuwa washauri wakuu wa mfalme
Alitarajia mmoja wao amuoe bintiye hoja yeyote iliyokamilika

(ii) Kwa nini Mfalme alishangaza na jawabu la binti yake (alama 2)
Mfalme alitarajia thamani ya tiba iwe kubwa
Kishaufu ni kitu duni

(c) "Akili ni nywele, kila mtu ana zake." Dhihirisha jinsi methali hii inavyobainika katika hadithi hii (alama 4)
1. Mwanakishwira alikuwa na akili bora kuliko mfalme/ wakwasi
2. Mchungaji alikuwa na akili nyingi kuliko mfalme
3. Mwanakishwira na mchungaji walikuwa na akili nyingi kuliko wakuasi na Mfalme
   Lazima pande zote mbili zilinganishwe wenye maarifa na wasio maarifa kila upande.

(d) Ni nini maoni yako kuhusu mwanaume aliyemwona mwanakishwira na kwa nini alikubali kuolewa na huyo. (alama 3)
1. Mwanaume hana taasubi ya kiume
2. Mchungaji ana akili sawa na Mwanakishwira
3. Mchungaji ndiye alitoa tiba ya ugonjwa wake
4. Mmoja alifumba fumbo (mwanakishwira) na mwingine akafumbua (mchungaji)
   Hoja yoyoye moja

http://atiaschool.org [0728 450 425]

(e) (i) Licha ya kuwa/ bali na/ zaidi ya kuwa/ juu ya hayo/ vile vile/ pia/ isitoshe/aidha/ kuongeza

(ii) Akilalamika/ alifura/ alihuzunika/ akisononeka/ akiwa na uchungu aliopita kiazi
(iii) Uzuri usio fifani/ wa ajabu/ mwingi sana
(iv) Akamshauri/ akampa mawaidha/ akamwasihi/ akamwangazia/ akamwambia/ akamwarifu

SWALI LA PILI

2 (a) (i) Alikuwa amewashinda wareno mahasimu wake na kwa hivyo wangendi kumwadhibu vikali
(ii) Ili Wareno wakija wakija wasikute chochote cha kuwavutia macho na watukomee kabisa
(iii) Hakutaka yaliyowapata wafaza yampate yeye na watu wake.
(3 x 2 = alama 6)

(b) (i) Faza alipoasi utawala wa Kireno aliangamizwa kinyama/ faza ilipoasi utawala wa Kireno Wareno waliangamiza chochote chenye uhai
(ii) Kila mreno hata kasisi aliunga mkono tokeo hili/ hakuna mreno hata mmoja aliyekilaani kitendo hiki.
(iii) Mfalme Yusuf baada ya kuwashinda Wareno aliwaamuru watu wake wahame aungamize mji ili wareno warudipo wasipate chochote cha kuwavutia.
(iv) Aliamua kuwashambulia Wareno katika vyao vyote katika mwambao mzima wa mashariki ya Afrika.
(v) Alienda Uarabuni kutafuta silaha
(vi) Alianza kuwashambulia Wareno kuko huko uarabuni kisha akaendelea kuwashambulia katika mwambao wa Afrika mashariki na kokote walikokuwa. (6 x 2 = alama 12)

SWALI LA TATU

3. (a) (i) Yule ndiye mkwasi aliyenusurika
(ii) Yule ndiye mkwasi ambaye alinusurika
(b) Andika umoja wa sentensi hizi
(i) Kwato za wanyama hutufaidi
Ukwato wa mnyama hunifadi (alama 1)
(ii) Mnataka vyeti vya kuwasaidia
Unataka cheti cha kukusaidia / kumsaidia (alama 1)
(c) Andika ukubwa wa:
(i) Mwizi aliiba kikapu na ng'ombe
Jizi liliiba kapu na ng'ombe/ jizi liliiba jikapu na jing'ombe (alama 2)
(d) Tunga sentensi sahihi ukidhihirisha wingi wa majina yafuatayo
(i) Ukanda
(a) Uzi au mshipi/ eneo ama sehemu Fulani/ wingi wake ni kanda (alama 1)

http://atikasecond.org 0728 450 425

(ii) Uzee
Hauna wingi wa uzee tu

(e) Sahihisha sentensi zifuatazo bila kugeuza maana
(i) Kikombe chenyewe kimevunjika ni kipya
(a) Kikombe kilochovunjika ni kipya/ kikombe chenye kuvunjika ni kipya/ kikombe
Kipya kemevunjika / kikombe kipya ndicho kilichovunjika (alama 1)
(ii) Nimepeana kitabu kwa mwalimu mkuu
(a) Nimempa mwalimu mkuu kitabu/ Nimempatia kitabu mwalimu mkuu (alama 1)

(f) Tunaweza kusema katika chumba au
(i) Chumbani
(ii) Ndani ya chumba

(g) Andika sentensi zifuatazo katika hali ya kutendewa
(i) Yule Ng'ombe alizaa ndama mkybwa jana (alama 2)
(a) Ndama mkubwa alizaliwa/ alizaliwa na ng'ombe yule jana
(ii) Mavu hawa wamemsumbua Nyatogo kwa muda mrefu
(b) Nyatogo amesumbuliwa na mavu hawa kwa muda mrefu (alama 2)

(h) Kwa kurejelea ngeli za mahali. Andika sentensi tatu ukionyesha matumizi ya kila moja (alama 3)
Hapo ndipo alipozaliwa (PO)
Huko ndiko alikozaliwa (KO)
Humo ndimo alimozaliwa (MO)

(i) Andika sentensi za mseto kutokana na mbili fupi ulizopewa
(i) Mwanafunzi amesoma- kwa bidii. Mwanafunzi anataka kupita mtihani (alama 1)
(a) Mwanafunzi anasoma kwa bidii ili apite mtihane. Pia kusudi / kwa kuwa anataka/ kwa vile anataka/ ndiposa/ ndipo/ maadama/ mathali n.k (alama 1)
(ii) Leo nimerudi nyumbani. Sipendi kuishi hapa
(a) Leo nimerudi nyumbabi ingawa sipendelei kuishi hapa. Pia ijapo/ ilipokuwa/ hata kama/ ingawaje/ ijapokuwa/ lakini n.k (alama 2)

(j) Geuza sentensi hizi kutoka msemo wa taarifa hadi msemo halisi
(i) Mama alisema nichukue nafaka yetu nikauze sokoni (alama 2)
(a) Mama alisema " chukua nafaka yetu ukauze sokoni"
(b) "Chukua nafaka yetu ukauze sokoni" mama akasema

(ii) Mwalimu aliomba aletewe vitabu vyake kutoka darasani (alama 2)
(a) "Nileteeni vitabu vyangu kutoka darasani". Mwalimu aliomba

http://atikaschool.org 0728 450 425